HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

# SHULE YA SEKONDARI PAWAGA

Simu:+255 714 421 782/0764 508 555 S.L.P 1184, Igodikafu-Pawaga
Baruapepe;pawagasecondaryschool@gmail.com IRINGA, TANZANIA

Kumb. Na.PSS/JI/2022/01 30/05/2022

JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………..
SHULE YA SEKONDARI ………………………………………………..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI PAWAGA WILAYA YA IRINGA MKOA WA IRINGA MWAKA 2022/2023

## 1.0 UTANGULIZI.

Ninafurahi kukutaarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano tahasusi ya…………… katika shule hii mwaka 2022. Shule ipo umbali wa km 60 kaskazini magharibi mwa mji wa Iringa katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

Usafiri wa basi kutoka Iringa mjini unapatikana stendi kuu ya mabasi ya mkoa wa Iringa.Panda mabasi yaendayo Pawaga na teremka njia panda ya Usolanga.Nauli ni sh.4000/= na usafiri unapatikana kila siku kati ya saa nne asubuhi hadi saa saba mchana.

Muhula wa masomo unaanza tarehe ………………….. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……………………. na mwisho wa kiripoti ni tarehe.

## 2.0.MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

### 2.1: SARE

a) Sketi mbili rangi ya kijani jeshi mshono linda box bapa ndefu .(sampli ya kitambaa imeambatanishwa)



b) Mashati mawili meupe ya mikono mirefu
c) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba na kung’arishwa kwa kiwi kikanyagio kifupi
d) Soksi nyeupe ndefu zisizo na urembo
e) Mavazi ya michezo(Track suti rangi ya dark blue)

f) Taulo moja
g) Jozi mbili za kitenge au kanga
h) Sweta rangi ya kijani (shingo ya V)
i) Hijabu ifanane na rangi ya shati la shule.
j) Sare ya kushindia (after classes dress) gauni rangi ya dark blue isiyobana mwili
k) Tai (ifanane na kitambaa cha sketi)

NB.KWA WANAFUNZI NA WAZAZI WATAKAOPATA SHIDA YA RANGI SARE HIZI WATAZIPATA SHULENI.

N.B MWANAFUNZI ASIJE NA MAVAZI MENGINE ZAIDI YA YALE YALIYOTAJWA

2.2: Mwanafunzi anaporipoti awe na vitu vifuatavyo.

1 Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko
2 Jembe moja lenye mpini
3 Fagio moja ngumu(hard bloom),fagio moja laini(soft bloom) fagio la kukaushia maji(squeezer),kwanja moja. 4 Fail moja(forder file) 5 Rim moja ya karatasi.
6 Godoro la futi sita na inchi mbili na nusu na mto
7 Shuka mbili rangi ya pink na blue
8 Chandarua
9 Daftari (counter books) kuanzia 10 pamoja na mkoba/ Begi la kubebea
10 Vitabu kulingana na tahasusi uliyopangiwa
11 Vyombo vya chakula
12 Tochi moja ya betri au solar itakayotumika kukiwa na tatizo la mwanga 13 Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia.
14 Scientific calculator
15 Mahitaji mengine binafsi ya kike na kiuanafunzi

N.B; NI MARUFUKU KWA MWANAFUNZI KUJA NA SIMU YA MKONONI.

3.0. Ada na michango

Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= au shilingi 35,000/= kwa muhula.fedha hizo zilipwe benki NMB kwenye akaunti namba 6051100059 Pawaga sekondari.Mwanafunzi aje na karatasi ya malipo ya benki(BPS) yenye jina lake.HAKUNA MALIPO YA ADA YATAKAYOFANYIKA SHULENI.

b)Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni

- Ukarabati wa samani 15000/=
- Kitambulisho na picha shilingi 6,000/=
- Taaluma shilingi 30,000/=

- Ulinzi na Mpishi shilingi 30,000/=
- Huduma ya kwanza 10,000/=
- Fedha ya tahadhari shilingi 5000/=
- Nembo ya shule shilingi 2000/=
- Mitihani ya kujipima shilingi 20000/=

JUMLA YA MICHANGO NI SH 118,000/= KWA MWAKA AU NI SH 59,000/= KWA MUHULA

Michango hii ilipwe kwenye Akaunti ya Shule Namba 6051100059 Shule ya Sekondari Pawaga katika benki ya NMB. Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye karatasi ya malipo ya benki (BPS) na aje nayo siku ya kuripoti.

NB.

1. Kwa mwenye kadi ya bima ya afya NHIF aje nayo kurahisisha huduma ya matibabu.
2. Gharama za matibabu Zaidi ya zile zinazochangiwa shuleni zitalipwa na mzazi.
3. Shule haina huduma ya chakula maalum(special diet)kwa wenye mahitaji hayo.

## 4.1: Sheria na kanuni za shule.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Namba 10 ya Mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kiripoti shuleni.

- i Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- ii Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni lazima
- iii Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- iv Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa hapa shuleni
- v Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka
- vi Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
- vii Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- viii Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- ix Kutunza mali za umma.
- x Kuwa na nywele fupi na za kupendeza.

## 4.2:Makosa yatakayosababisha kufukuzwa shule mwanafunzi.

- Wizi
- Uasherati,uhusiano wa jinsia moja

- Ubakaji
- Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli nk
- Kupigana au kupiga,
- Kuharibu kwa makusudi mali ya umma,
- Kupata mimba au Kutoa mimba
- Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule na watu
- Kumiliki au kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
- Kudharu bendera ya taifa.
- Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
- Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
- Kushirki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
- Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
- Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika.wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
- Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
- Kutohudhuria masomo zaidi ya siku tisini bila taarifa/utoro.

Tabia njema ni lazima na inatiliwa mkazo hapa shuleni.Mwanafunzi mwenye tabia mbaya hafai kupewa elimu ya sekondari au hata elimu ya juu.Ni lazima mwanfunzi awe na tabia nzuri na kufuata taratibu za shule pia kuwatii wafanyakazi na walimu wengine wenye mamlaka.Heshima kwa mtu yeyote mwenye mamlaka ni kitu cha lazima. Unatakiwa  kuvaa sare ya shule kwa mshono unaokubaliwa na taratibu za shule zinavyoeleza hasa wakati wa

1. Masomo darasani
2. Safari za nje ya shule kwa jina la shule ikiwa ni pamoja na kwenda likizo
3. Kwenda hospitali
4. Maandamano ya amani

Mwisho kabisa natumia nafasi hii tena kukukaribisha sana hapa Pawaga sekondari na ni matarajio yangu kuwa ufikapo hapa utatumia vema fursa hii muhimu uliyotunukiwa na taifa lako kwani wengi wameikosa.

Unakaribishwa sana Shule ya Sekondari Pawaga

Jairos Edward Mwakavindi

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

# SHULE YA SEKONDARI PAWAGA

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA TANO**

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI PAWAGA,
S.L.P 1184,
**IRINGA**

MWANAFUNZI (SEHEMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE)

Mimi ……………………………………………………………………………………………….

Nimesoma kwa makini barua ya maagizo ya kujiunga na shule yako na sheria zake.Kwa heshima na unyeyekevu mkubwa nakubali/sikubali nafasi hiyo kwa sababu……………………………………….

Pia nayakubali/siyakubali masharti/sheria za shule yako.

MZAZI/MLEZI (SEHEMU HII IJAZWE NA MZAZI AU MLEZI)

Mimi ……………………………………………………………………….. mzazi/ mlezi wa ……………………………………………….. Ambaye amechaguliwa kujiunga na shule yako, nimesoma maagizo ya kujiunga na shule na pia sheria zake.Ninakubali/sikubali nafasi hiyo(Kwa anayekubali).Ninaahidi kumtimizia mtoto wangu maagizo yote ya kujiunga na shule hiyo katika muda uliopangwa.Pia nitashirikiana daima na shule yako katika kumkuza na kumlea mtoto wangu.

Ahsante.

Jina mzazi/ mlezi ………………………………………………….

Anuani yake……………………………………………………….

Mtaa/Kitongoji anapoishi………………………………………… Sahihi

……………………………………..

Tarehe ……/ ……/ 2022.

HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

# SHULE YA SEKONDARI PAWAGA

FOMU YA KUPOKELEWA SHULENI.

1. Jina kamili…………………………………………………………………………………………………………………… 2. Mahali ulipozaliwa ……………………………………………………………………………………………………..

3. Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………………………………………………………………….. 4. Anuani ya nyumbani…………………………………………………simu…………………………………………..

5. Jina la mzazi/mlezi………………………………………………………………………………………………………

6. Anuani ya mzazi/mlezi(kama tofauti na hiyo hapo juu)……………………………………………….....
…………………………………………………..kazi yake…………………………………………………………………

7.Mzazi/mlezi/ ndugu wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni(wawe na kitambulisho chochote wanapokuja)

| | Jina | uhusiano | anuani yake | simu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ……………………………….. | ………………………… | ……………………………. | ………………………………. |
| 2. | ……………………………….. | ………………………… | ……………………………. | ………………………………. |
| 3. | ……………………………….. | ………………………… | ……………………………. | ………………………………. |
| 4. | ……………………………….. | ………………………… | ……………………………. | ………………………………. |

8. Jina…………………………………………………………………………………………………………………………….

9.Kidato ulichopokelewa……………………………………………………………………………………………….

10.Shule uliyotoka…………………………………………………………………………………………………………

11.Namba ya mtihani wa kidato cha nne………………………………………………………………………………

12.Shughuli unazopendelea mbali na masomo kama vile mpira wa miguu,mpira wa mikono Mpira wa pete,riadha,kuimba n.k………………………………………………………………………………......

13.Wilaya unakotoka…………………………….kata……………………………mtaa…………………………………

14.Nikihama nitatoa taarifa

PAWAGA SECONDARY SCHOOL.MEDICAL EXAMINATION FORM

(**To be completed by medical officer in respect of all new students)**

Student's full name…………………………………………………………………………….Age……………………………

1.Bloodcount(red and white)………………………………………………………………………………

2.Urine examination……………………………………………………………………………………………….

3.Stool………………………………………………………………………………………………………………….

4.Syphilis……………………………………………………………………………………………………………..

5.T.B……………………………………………………………………………………………………………………

6.Ear test……………………………………………………………………………………………………………..

7.Eye…………………………………………………………………………………………………………………..

8.Spleen………………………………………………………………………………………………………………

9.Pregnancy test…………………………………………………………………………………………………..

10.Abdomen…………………………………………………………………………………………………………

11.Additional information or any other physical, mental, hereditary of infectious diseases……………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………………..

Treatment after examination……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………

Medical certificate

I certify that the above concerned has been examined and found fit/unfit to join high school education.

Signature……………………………….Designation…………………………..Station……………………………………….

(Official stamp) Date ………/……../20…..

NB.

1. Fomu hii ijazwe na mganga katika hospitali inayotambulika na serikali.
2. Mwanafunzi hatopokelewa ikiwa hajakamilisha fomu hii

ORODHA YA VITABU VYA MASOMO (mzazi unaweza ukamnunulia mwanao angalau kitabu kimoja kwa kila somo)

**PHYSICS**

1. Nelkon and parker, advanced level physics 7th edition
2. S.chands principles of physics class XI
3. S chands principles of physics ,class XII
4. Jim breithaupt, understanding physics 2nd /4th edition
5. Roger monastery, Advanced Level physics 4th edition
6. Tom Duncan, Advanced level physics
7. University Physics, New Edition

**CHEMISTRY**

1. Physical chemistry, by Delungu ( Mzumbe bookshop project 1998)
2. Advanced inorganic chemistry part I and II (Tanzania Institute of Education)
3. Organic chemistry part I , the fundamental principles I.L (Longman LTD)

**GEOGRAPHY**

1. Principles of physical geography by F. J monk house 2. Geography intergrated approach by D. Waugh
3. Essentials of Practical Geography by josephat Mwita
4. General geography in diagrams by R.B burnet
5. Simplified physical geography (A-LEVEL ) by D.M
6. Statistical methods and the geographers by S. Gregory

**BIOLOGY**

1. Biological Science; Cambridge University press 1997 3rd edition
2. Functional approach by MBv Robert
3. New Understanding Biology By Suzan Toole
4. Advanced biology principles and application By C.J Clegg and Mackean
5. Advanced biology by Michael Kent (2000) 0xford Unversity Press uk
6. Biology class XI and XII S. Chands

**ADVANCED AND BASIC APPLIED MATHEMATICS**

1. Basic Applied Mathematics by Kiza and Septine I sillem
2. Advanced Mathematics by Shayo
3. Advanced Mathematics book 1 and 2 by Backhouse
4. Advanced Mathematics CHANDS 1 and 2
5. TRANTER
6. Pure mathematics 1 and 2

**GENERAL STUDIES**

1. General studies for A- level certificate form v

2. Contemporary approach for A-level general studies notes for form v and six
3. General studies supplementary book for A-level and colleges

**ECONOMICS**

1. Economics Theory by Gupta
2. Micro-economics by Dwiverd
3. Economic simplified by N A Saleemi
4. Modern economics By Robert Mudida